# TUZO YA TAIFA YA MWALIMU NYERERE YA UANDISHI BUNIFU
# MWAKA WA NNE - 2025/2026

## VIGEZO

### VIGEZO VYA JUMLA KWA NYANJA ZOTE

- **Mshiriki awe raia wa Tanzania.**
- **Andiko bunifu liwe katika lugha ya Kiswahili.**
- **Sehemu yoyote ya mswada isiwe imechapishwa na mchapishaji au kuchapishwa binafsi pamoja na kuchapishwa mtandaoni na magazetini, au kurushwa katika vyombo vya habari na burudani au kuoneshwa jukwaani.**
- **Mwandishi anaruhusiwa kushiriki andiko bunifu moja tu katika nyanja atakayochagua.**
- **Mswada utakaoshinda tuzo nyingine hautazingatiwa.**
- **Andiko bunifu litakalowasilishwa liwe andiko makini lililojikita katika masuala muhimu ya jamii.**
- **Miswada iliyoshika nafasi ya 1 - 10 katika tuzo ya miaka iliyopita haitaruhusiwa kushiriki. Hata hivyo, mwandishi anaweza kuleta mswada mwingine.**

### VIGEZO MAHSUSI KWA TAMTHILIYA

- **Andiko litumie “Courier font”, ukubwa wa herufi uwe 12.**
- **Mswada uwasilishe wazo asili la mwandishi.**
- **Mswada utumie vionjo vya sanaa za maonyesho za Kitanzania.**

- **Mwandishi aainishe muswada wake ni Tamthiliya ya aina gani.**

**TAMTHILIYA YA JUKWAANI;**

- **Tamthiliya iwe ya muda wa dakika 40 hadi 60.**
- **Tamthiliya iwe na maonyesho yasiyozidi 6.**
- **Wahusika katika tamthiliya wasizidi 6.**

**TAMTHILIYA YA RUNINGA;**

- **Tamthiliya iwe na "episodi" 13.**
- **Kila "episodi" katika tamthiliya iwe ya muda usiozidi dakika 30.**

**TAMTHILIYA YA REDIO;**

- **Tamthiliya iwe na "episodi" 13.**
- **Kila "episodi" katika tamthiliya iwe ya muda usiozidi dakika 30.**
- **Wahusika katika tamthiliya wasizidi 7.**

## VIGEZO MAHSUSI KWA RIWAYA

- **Urefu wa riwaya uwe kati ya maneno 60,000 na 100,000.**
- **Andiko litumie "Times New Roman", ukubwa wa herufi uwe 12 na "double spacing"**

## VIGEZO MAHSUSI KWA HADITHI ZA WATOTO

- **Hadithi ya watoto iwe kati ya maneno 250 na 1,000 .**
- **Hadithi itakayowasilishwa ilenge watoto wa miaka 5 hadi 12.**
- **Mwandishi aainishe hadithi yake imelenga watoto wa umri gani.**

- **Mswada utakaowasilishwa ujumuishe michoro. Kila mchoro uendane na maudhui ya hadithi.**
- **Mswada utumwe kama PDF.**
- **Hadithi itakayowasilishwa itumie lugha rahisi inayoeleweka.**

## VIGEZO MAHSUSI KWA USHAIRI

- **Mashairi yasipungue 50 na yasizidi 60. Idadi ya beti kwa kila shairi isizidi 15. Pia, ikiwa mswada ni wa utenzi , uwe utenzi mmoja tu na uwe na beti kati ya 300-400.**
- **Kila shairi lipewe namba.**
- **Andiko litumie "Times New Roman", ukubwa wa herufi uwe 12.**

## TARATIBU ZA KUWASILISHA MISWADA:

- **Andiko bunifu litumwe kama kiambatisho kwa Microsoft Word kwa miswada ya Ushairi na Riwaya; PDF kwa Hadithi za Watoto; na FDX au PDF kwa Tamthiliya.**
- **Kwa wale wenye mahitaji maalumu wanaweza kutumia Nukta Nundu.**
- **Kiambatisho kiwe na jina la andiko bunifu na nyanja aliyoiandikia.**
- **Ukurasa wa kwanza wa andiko bunifu uwe na kichwa cha andiko bunifu na jumla ya maneno au idadi ya beti kwa ushairi.**
- **Andiko bunifu liwe na namba kwenye kila ukurasa.**
- **Mwandishi asiandike jina lake wala taarifa binafsi kwenye andiko bunifu.**
- **Mwandishi aweke taarifa zifuatazo kwenye barua pepe itakayoambatana na mswada wake: Majina**

**matatu, jina la uandishi (kama analo), Jinsia, namba ya simu, anuani, wasifu usiozidi maneno 150 na umri. Mwandishi asiweke taarifa hizi kama kiambatisho.**

- **Kila mshiriki atatakiwa kusaini tamko la kuthibitisha kuwa muswada huo ni wake na haujachapishwa mahali popote ikiwemo mtandaoni na magazetini.**
    - **Tamko linapatikana kupitia https://bit.ly/TAMKOTUZO2025**
- **Andiko bunifu liwasilishwe kati ya Agosti 15 na Novemba 30, 2025.**
- **Mawasilisho yote yatumwe kwa tuzonyerere@tie.go.tz**

**MISWADA ITAKAYOSHINDANISHWA NI ILE ILIYOZINGATIA VIGEZO. TAFADHALI HAKIKISHA UNAFUATA VIGEZO VYOTE KAMA VILIVYOAINISHWA.**